Tanzania Child Rights Forum

"together for a lasting positive change for children"

TAMKO LA JUKWAA LA HAKI ZA WATOTO (TCRF) KUHUSU HAKI ZA WATOTO KATIKA KATIBA MPYA

Marekebisho ya 23 January 2013

YALIYOMO *KURASA*

TAMKO LA JUKWAA LA HAKI ZA WATOTO (TCRF) 0
KUHUSU HAKI ZA WATOTO 0
KATIKA KATIBA MPYA 0
1.2 Madhumuni ya waraka huu 3
1.3 Mbinu zilizotumiwa wakati wa ushiriki wa mchakato wa Katiba 3
1.4 Umuhimu wa Ibara zinazohusiana na Haki za Watoto katika Katiba 3
1.4.1 Dhana ya Katiba kama sheria mama na umuhimu wake katika haki za watoto 3
1.4.2 Nafasi ya watoto kama kundi kubwa katika idadi ya watu katika Tanzania 4
1.4.3 Nafasi Ya Watoto Kama Kundi Linalohitaji Uangalizi Maalum 5
1.4.4 Nafasi ya Serikali ya Tanzania kama Msimamizi wa Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda kuhusu Watoto 5
1.4.5 Umuhimu wa kuwa na Katiba kama Kiungo na Kichocheo cha Kutunga Sera na Sheria Endelevu zinazowahusu Watoto 6
2. KANUNI ZA MSINGI ZINAZOPASWA KUZINGATIWA WAKATI WA UANDIKAJI WA VIPENGELE VYA KATIBA VINAVYOHUSIANA NA WATOTO 7
2.1 Kuweka Mbele Maslahi ya Mtoto (Best Interests of Child Standards) 7
2.2 Kuepuka na Kuondoa Ubaguzi 8
2.3 Kushirikisha Watoto na Haki ya Kusikilizwa na Kuheshimu Mtazamo wa Mtoto) 10
2.3.1 Umuhimu wa Haki ya Mtoto ya Kusikilizwa. 10
2.3.2 Haki ya Mtoto Kushirikishwa Inahusisha nini? 11
2.3.3 Umuhimu wa kumpatia mtoto haki ya kushiriki 12
2.3.4 Athari ya kutomsikiliza mtoto na kutozipa umuhimu hoja wanazotoa 12
2.3.5 Faida ya Kuwasikiliza Watoto na Kupokea Mawazo na Hoja zao 13
3. 0 HAKI MAHSUSI ZA WATOTO ZINAZOPASWA KUZINGATIWA KATIKA KATIBA MPYA 15
3.1 Haki ya kuwa na Utambulisho (kuwa na Jina, Utambulisho wa Utaifa na kuwatambua) 15
3.2 Haki ya Afya na Haki ya Kuishi 16
3.3 Haki ya Kupata Elimu 18

3.4 Haki ya Kutoa Maoni 18

3.5 Haki ya kuwa na Mfumo Rafiki wa Haki kwa Watoto walio katika Ukinzani na Sheria 19

3.6 Haki ya kulindwa dhidi ya uonevu, ukatili na udhalilishaji..... 21

3.8 Kuundwa kwa Taasisi Maalum ya Kuratibu, Kusimamia na kufuatilia Utekelelezaji wa Haki za Watoto Nchini 22

3.9 Mfumo wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto..... 22

3.10 Kumomonyoka kwa maadili katika Jamii..... 22

Kiambatanisho cha Masuala muhimu yanayowahusu Watoto 24

1.1 Utangulizi

Mwaka 2010, Tanzania ilitangaza kuanza mchakato wa kuandika Katiba mpya kuitikia mwito wa muda mrefu wa watu wa makundi mbalimbali waliodai kuandikwa kwa Katiba mpya. Kama ilivyo kwa nchi nyingine za Kiafrika michakato ya kuandika Katiba inategemea zaidi matakwa ya wakati husika na hali halisi ya mazingira ya kijamii , kiuchumi na kisiasa. Kama inavyofahamika na wengi Katiba ni msingi ambamo kwayo taasisi mbalimbali za utawala zinapata mamlaka na nguvu ya kutekeleza majukumu yao na pia ndio chanzo cha sheria zote za nchi.Hivyo kuifanya Katiba kuitwa sheria mama kwa kuwa Katiba huelezea malengo na matazamio ya nchi na namna nchi ianavyotaka kujiongoza katika kufikia malengo kama taifa.

Kwa Tanzania hii ni nafasi adhimu ya kuunda Katiba mpya baada ya zaidi ya miaka 35 ya Katiba ya sasa ya mwaka 1977 ambayo imefanyiwa marekebisho mbalimbali ili kukidhi matakwa ya jamii iliyopo. Kihistoria mchakato huu wa kuandika Katiba mpya mara ya ya sita. Mara tano zilizotangulia zilifanyika ndani ya kipindi kifupi sana tangu tupate uhuru na zilifanyika ili kuiwezesha Tanzania kukabiliana na changamoto za kuwa taifa huru.

Pamoja na ukweli kwamba Katiba ni jambo linalowagusa watu wote nchini Tanzania, kumbukumbu zinaonyesha ushiriki wa wananchi katika uandikaji wa Katiba zilizopita haukuwa wa moja kwa moja. Kwa kiasi kikubwa ushiriki huo ulitawaliwa na kusimamiwa zaidi na vyombo vya utawala, tofauti na malengo na misimamo ya kanuni za kidemokrasia na utawala bora zinazotaka kuwepo na ushirikishwaji wa makundi mbali mbali ya kijamii ili kuhakikisha Katiba inayopatikana inabeba matazamio ya watu na inaleta matunda yanayotarajiwa kwa watu wote. Hali hii haikuwepo katika uandikaji wa Katiba zilizopita kwa kukosa ushiriki wa wananchi moja wa moja na hivyo kuwafanya watu wengi kuhoji maudhui yake.

Jukwaa la Haki za Watoto Tanzania (Tanzania Child Rights Forum -TCRF) ambalo linaratibu mashirika yasiyo ya kiserikali zaidi ya 100 yanayotetea haki za watoto Tanzania Bara kama zilivyoainishwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989 (CRC) na Mkataba wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa Afrika wa mwaka 1990(ACRWC), Sheria ya Mtoto 2009 na Sera ya Mtoto ya mwaka 2008 umeonyesha nia ya kuwa mmoja wa wadau katika mchakato wa kuandika Katiba mpya.

Kwa mantiki hiyo basi, iliazimiwa kuwa TCRF kwa niaba ya wanachama wake ichukue jukumu la kuratibu, kuandaa na kuwasilisha maoni ya wanachama wake wakati wa mchakato wa kuandika Katiba mpya kwa kuandaa maoni yatakayohakikisha kanuni na haki za msingi zenye kuhusiana na ulinzi na ustawi wa mtoto zinaingizwa katika Katiba mpya kama zilivyokubaliwa na Tanzania katika mikataba ya kimataifa na sera na sheria za nchi.

1.2 Madhumuni ya waraka huu

Madhumuni makubwa ya ushiriki wa TCRF katika mchakato wa kuandika Katiba mpya ni kushawishi kuwepo kwa Katiba ambayo inatambua na kuweka masharti ya msingi yanayohusiana na haki za watoto kwa lengo la kulinda na kustawisha haki za watoto katika taifa la Tanzania.

1.3 Mbinu zilizotumiwa wakati wa ushiriki wa mchakato wa Katiba

Mojawapo ya mbinu iliyotumiwa sana ni kuhakikisha asasi za kijamii ikiwa ni pamoja na zile zinazoongozwa na watoto na vijana ambazo ni wananchama wa TCRF na nyinginezo ambazo si wanachama lakini zinaamini katika ustawi wa haki za watoto; zinapata fursa ya kushiriki katika mchakato wa kuandika Katiba zikiwa na lengo kuu la kuhakikisha kuwa haki za watoto zinazingatiwa katika Katiba mpya.

Njia nyingine iliyotumiwa na TCRF ni kuwawezesha watoto na vijana kupitia vyama au jumuiya zao kushiriki katika mchakato kwa kutoa maoni. Kwa minaajili hiyo TCRF imefanya kazi kwa karibu na mabaraza ya watoto yanayosimamiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na yale yanayosimamiwa na asasi za Save the Children na Plan Tanzania ambayo yameundwa karibu nchi nzima.

Njia nyingine iliyotumiwa ni kuhakikisha kunakuwa na ushirikiano wa hali ya juu na mashirika mengine ambayo yamekuwa yanashiriki mchakato huu, kama vile Jukwaa la Katiba; Kamati ya Katiba ya Chama cha Wanasheria wa Tanganyika; Kigoda cha Mwalimu Nyerere cha Kikuu cha Dar es Saalaam, Jukwaa la Jinsia linalosimamiwa na Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA), Muungano wa Wanaharakati wa Haki za Wanawake (FEMACT) na baadhi ya Taasisi za elimu ya juu.

1.4 Umuhimu wa Ibara zinazohusiana na Haki za Watoto katika Katiba

1.4.1 Dhana ya Katiba kama sheria mama na umuhimu wake katika haki za watoto

Dhana ya kuitazama Katiba kama sheria mama ina maana kubwa katika nchi. Kwa kifupi inamaanisha kuwa Katiba ndio sheria kuu ya nchi ambayo kwayo sheria na taratibu mbalimbali za uendeshaji wa dola zinatokana nayo. Dhana hii inamaanisha kuwa mamlaka ya serikali katika kutekeleza majukumu yake lazima yawe na uwiano na matakwa ya Katiba. Serikali isiyofuata matakwa haya inaonekana kuwa ni serikali isiyofuata misingi ya kidemokrasia.

Kwa mustakabali huu serikali inayofuata matakwa ya Katiba ni ile inayotambua umuhimu na nafasi ya mahakama katika kutoa haki na kutafsiri sheria na uwezo wa kutangaza na kufuta

vipengele vyovyote vya sheria yoyote iliyopitishwa na bunge endapo vipengele hivyo vinakiuka Katiba.

Katiba mara nyingi huweka misingi ya kutunza na kusimamia haki na uhuru wa wananchi ambayo inapaswa kulindwa na kuheshimiwa na mamlaka za nchi. Kwa msingi huu Katiba huwa ni mkataba usiotarajiwa kubadilishwa mara kwa mara na ibara zake huwekewa masharti magumu ya ubadilishwaji au urekebishwaji wake na mara nyingi kanuni hizi za ubadilishwaji huwa ni ngumu na lazima zikubalike na wadau wote waliohusika katika kuitunga.

Dhana ya Katiba kama sheria mama pia huzingatia Falsafa ya Demokrasia ya Katiba badala ya demokrasia ya kibunge. Katika dhana hii demokrasia hupimwa kutokana na ukuu wa Katiba(Constitutional Supremacy) unavyoheshimiwa tofauti na demokrasia ya kibunge ambayo hukazania zaidi ukuu wa bunge (Parliamentary Supremacy) dhidi ya Katiba. Kutokana na dhana hiyo, TCRF inaona umuhimu wa Katiba ya nchi kuwa na ibara zinazozungumzia haki za watoto ili haki hizi ziwe na nguvu ya kudumu ya kiKatiba isiyoweza kubadilika kwa matakwa ya wachache. Umuhimu huu pia umesisitizwa na Kamati ya Kimataifa ya Haki za Mtoto katika tamko lake Namba Tano (5) ilipendekeza:

> *Haki zinazotolewa kwa watoto ziwe ni haki ambazo zinaweza kusimamiwa na mahakama. Kamati inakaribisha uwezekano wa kuingizwa kwa ibara za haki za watoto katika Katiba za nchi kama zilivyoainishwa katika mikataba ya kimataifa zinazoweka msisitizo kuwa watoto kama ilivyo kwa watu wazima wanazo haki za binadamu.*

Tamko hili pia lilitambua kuwa kufanywa kuwa haki ya kiKatiba pekee hakutoshi kuzifanya haki hizo ziheshimiwe bali lilisisitiza umuhimu wa kutunga sheria na kanuni mbalimbali zitakazohakikisha haki hizi za watoto zinalindwa na kuheshimiwa ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo watoto wenyewe kudai na kulinda haki zao pamoja na kutimiza. Hivyo basi kuingiza ibara za haki za watoto katika Katiba ni muhimu ili kuweka msingi wa kutunga sheria nyingine zinazoimarisha haki, ulinzi na usalama kwa watoto.

1.4.2 Nafasi ya watoto kama kundi kubwa katika idadi ya watu katika Tanzania

Sababu nyingine inayotushawishi kusisitiza umuhimu wa kuwa na ibara za Katiba zinazoangalia haki za watoto ni nafasi ya watoto kama kundi muhimu na kubwa katika nchi. Kwa mujibu wa takwimu za awali za Sensa ya Watu na Makazi (2012 Tanzania ina watu Milioni 44.9 ambao kati yao asilimia zaidi ya 50 (50%) ni watoto. Hivyo mchakato huu wa kuandika Katiba mpya ni nafasi adhimu kwa Tanzania kuonyesha inajali na kuthamini kundi hili kubwa na muhimu la wananchi wake ambao wana umri chini ya miaka 18.

Malezi na makuzi bora ya watoto hujenga taifa bora kinyume chake ni kujenga kizazi kisichojitambua na kuwajibika katika kuchangi maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika taifa letu la Tanzania. Hivyo basi ni muhimu kutambua kuwa Tanzania kama nchi yoyote ili iweze kufikia malengo yake ya kimaendeleo haiwezi kukwepa jukumu la kuwaandaa watoto

kwa kuweka mazingira bora ya kuwawezesha kuwa raia wenye mchango kwa maendeleo ya nchi yao.

Inategemewa pia watakuwepo watu wakati wa mchakato huu watakaodai kuwa haki za binadamu zinawajumuisha watoto. Kwa kutambua hilo waraka huu wa maoni umejikita zaidi katika haki za kimsingi na zinazowagusa watoto moja kwa moja kama kundi maalum na hizi ndizo TCRF inapendekeza ziingie katika Katiba. Lengo hasa la kufanya hivi ni kuzihuisha haki hizi na kuzipa uwezo wa kuzidai katika mahakama zetu na hivyo kuwapa wadau nafasi ya kuzidai pale zinapokiukwa au zinaposhindikana kutekekelezwa.

1.4.3 Nafasi Ya Watoto Kama Kundi Linalohitaji Uangalizi Maalum

Pamoja na kutambua kuwa haki za binadamu kwa ujumla zinawagusa watoto pia ni muhimu kufahamu kuwa watoto wanahitaji ulinzi wa ziada kutokana na hali yao na namna wanavyoguswa na ukiukwaji wa haki zao na unayanyasaji. Kwa mujibu wa taarifa ya utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto (Violence Against Children - VAC) uliofanyika Tanzania mwaka 2009, watatu kati ya wasichana 10 na mmoja kati ya wavulana saba hunyanyaswa kijinsia kabla ya kutimiza miaka 18. Utafiti huu pia ulionyesha kwamba robo ya watoto wote walioko Tanzania wanakumbana na unyanyasaji wa kihisia (emotion) ambapo watoto yatima walionekana kunyanyaswa zaidi ya wasiokuwa yatima[1]. Kwa upande wa unyanyasaji wa kimwili zaidi ya asilimia 75 ya watoto wameathiriwa na hali hii.

Kwa sababu ya unyonge wao na uwezo wao mdogo wa kujilinda wao wenyewe na kukabiliana na changamoto hizi watoto wanahitaji Katiba itakayowalinda kwa kuhakikisha kuwa inatoa mamlaka ya kutunga sheria za kuwalinda.

Jambo hili linatiliwa mkazo zaidi na utegemezi wa Watoto kwa watu wazima kusimamia na kulinda haki zao pale zinapokiukwa kwa kuwa watoto kwa sababu ya unyonge wao, na ukosefu wa fursa kwa wao kushiriki na kushirikishwa katika kufikia maamuzi katika jamii zao yanayogusa haki zao. . Hivyo inatarajiwa kuwa Katiba itakayoandikwa itatoa nafasi kwa haki za watoto kupewa uzito unaostahili.

1.4.4 Nafasi ya Serikali ya Tanzania kama Msimamizi wa Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda kuhusu Watoto

Tanzania pia inabanwa na matakwa ya kuheshimu misimamo na makubaliano ya Kimataifa ambayo imeyaridhia . Tanzania ilisaini Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (Convention on the Rights of the Child - CRC) mwaka 1991 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa WMtoto (African Charter on the Rights and Welfare of the Child - ACRRWC) wa mwaka 2003. Tanzania pia imesaini Itifaki ya Hiari kuhusu Usafirishaji Watoto, Ukahaba wa Watoto na

[1] Kwa Maelezo zaidi soma UNICEF (2011)Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania. Matokeo ya Utafiti wa Kitaifa, 2009: Muhtasari wa Kuenea kwa Ukatili wa Kijinsia, Kimwili na Kiakili, Muktadha wa Matukio ya Ukatili wa Kijinsia, Afya na Athari ya Tabia Kwa Ukatili Uliyotokea Utotoni, Dar es Salaam, Tanzania",

picha za Ngono wa mwaka 2003 na Itifaki ya Hiari Kuhusu Kupiga Marufuku Kuwahusisha Watoto katika Vita ya mwaka 2004. Pia ilisaini Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi kwa Wanawake na Watoto (CEDAW). Mikataba yote hii inahimiza kutoa nafasi makundi maalum.

Kwa upande wa haki za watoto, mkataba wa CRC na ule wa ACRWC unazitaka serikali kuchukua hatua muhimu za kisheria, kiutawala na nyinginezo ili kuwaepusha watoto dhidi ya unyanyasaji wa kimwili na kiakili; maumivu au mateso na kutokuwajali watoto, kuwatesa au kuwadhalilisha kingono.

Katiba inayoandikwa ina wajibu wa kutambua waziwazi haki za watoto kama zilivyotambuliwa na Tanzania kwa kusaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kikanda na Kimataifa. Kujumuishwa kwa haki hizi za watoto katika Katiba itakuwa pia ni uthibitisho kuwa Tanzania haikusaini mikataba hii kwa nia ya kuwafurahisha wadau wake wa kimataifa bali kuwa na nia ya dhati ya kuhakikisha inaweka mazingira yakinifu ya kutekeleza haki hizi.

Kwa kuingiza haki hizi za watoto Tanzania itakuwa inajiunga na baadhi ya nchi za kiafrika zilizoamua kuingiza haki za watoto katika Katiba zao kama nchi ya Kenya mwaka 2010, Uganda mwaka 1995 na Afrika Kusini mwaka 1996. Kuingizwa kwa haki hizi katika Katiba za nchi hizi kumesaidia sana kutunza haki za watoto hasa pale zinapovunjwa[2].

1.4.5 Umuhimu wa kuwa na Katiba kama Kiungo na Kichocheo cha Kutunga Sera na Sheria Endelevu zinazowahusu Watoto

Serikali ya Tanzania imepiga hatua kubwa kwa kuweka mazingira ya kuwa na sera na mfumo wa sheria unaojali haki za Watoto na namna ya kuzilinda. Hatua ya Serikali ya Tanzania kuanzisha mchakato wa mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008; kutunga Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 na kuanzisha Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa Watoto Waishio Katika Mazingira Magumu ni uthibitisho kuwa serikali ina nia njema ya kutambua umuhimu wa haki za watoto. Ni vyema pia kutambua kuwa Tanzania imekuwa nchi ya pili kwa Afrika baada ya Swaziland kufanya utafiti wa kina kuhusu ukatili dhidi ya watoto.

Pamoja na jitihada hizi TCRF inatambua kuwa bado safari ni ndefu hadi kufikia hali ya kuheshimu haki za watoto katika maeneo mengi kwa kuwa haki hizi hazina nguvu ya kiKatiba. Baada ya kufanya mapitio ya maendeleo ya Tanzania katika kufikia malengo ya Milenia ambapo imeonekana dhahiri kuwa hali sio ya kuridhisha sana, ijapokuwa kuna matumaini ya kufikia lengo namba 3 linalohusiana na elimu kwa wote. Ni vizuri kufahamu kuwa mengi ya malengo haya yanahusiana na ustawi na haki za Watoto. Malengo ya MDG yanapaswa kutimizwa mwaka 2015 na ni matarajio ya wengi kuwa baada ya 2015, ajenda au malengo mengine ya kidunia yatakayofuata, nayo pia yatahusisha haki za watoto.

[2] Katika sehemu inayofuata tutajidili kwa kina namna Katiba za nchi hizi zilivyoingiza haki za watoto katika Katiba zao ili kuonyesha namna ambavyo mchakato wa kutunga ktiba ya Tanzania utakavyoingiza haki za waototo katika Katiba hiyo.

Kwa sababu hizi TCRF inaamini kuwa hatua hii ya uandikaji wa Katiba mpya itatoa dira ya namna haki hizi za watoto zitaweza kulindwa kikatiba kwa kipindi pengine cha zaidi ya miaka hamsini ijayo, na hivyo inatoa fursa kwa Tanzania kuwa nchi ya mfano katika kuweka kanuni za kikatiba za ulinzi wa Watoto zenye kutoa mwelekeo wa namna malengo yafuatayo ya kidunia yanavyotakiwa kuwa.

Ikumbukwe pia kuwa Tanzania ni mojawapo ya nchi zilizoteuliwa na Umoja wa Mataifa kuongoza mjadala na majaribio ya ajenda kuu ya maendeleo ya Umoja wa Mataifa baada ya mwisho wa Malengo ya Milenia 2015. Hivyo ni dhamira ya TCRF kuikumbusha serikali ya Tanzania kuhakikisha kuwa masuala ya Watoto yanabakia kuwa masuala muhimu kuzingatiwa katika mijadala ya kuandaa ajenda ya kimataifa ya maendeleo. Fursa hii ya Katiba mpya ni muhimu sana kwa kuhakikisha Tanzania inaweka mazingira ya kuwezesha mijadala hiyo.

2. KANUNI ZA MSINGI ZINAZOPASWA KUZINGATIWA WAKATI WA UANDIKAJI WA VIPENGELE VYA KATIBA VINAVYOHUSIANA NA WATOTO

Katika sehemu hii TCRF inajaribu kuleta katika sehemu moja nguzo kuu za mijadala kuhusu haki za watoto kama zilivyochukuliwa katika muktadha wa mikataba ya kimataifa hasa mkataba wa CRC na ACRWC ambayo Tanzania imeridhia. Katika mtazamo wa haki za Watoto nguzo hizi ni muhimu kiasi kwamba haitegemewi nchi yeyote iliyosaini mikataba ya haki za watoto kuzikwepa.

TCRF inaamini kuwa nguzo zitakazojadiliwa katika sehemu hii ndizo pia zinatarajiwa ziwe nguzo kuu zitakazoingizwa katika uandikaji wa Katiba mpya. TCRF pia inaamini kuwa Nguzo hizi si ngeni kwa kuwa zimeainishwa katika mikataba ya kimataifa hasa ule wa CRC na ACRWC na pia umewekewa mkazo katika Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 na Sheria ya Haki za Mtoto ya Mwaka 2009.

Nguzo hizi zinazopendekezwa na asasi za kiraia zilizo katika mwavuli wa TCRF ni:

1. Kuweka mbele maslahi ya Mtoto
2. Kuishi na makuzi ya Mtoto
3. Kuepuka ubaguzi
4. Ushirikishwaji
5. Kutoa huduma stahiki
6. Na ulinzi wa Mtoto

Nguzo/misingi hii inapaswa kuwaongoza wananchi wote, Bunge, Serikali Kuu, Mahakama, Baraza la Mawaziri, Vyama vya Siasa na Taasisi nyingine katika kutekeleza sera mbalimbali zenye lengo la kujenga jamii huru inayojali haki na maslahi ya Watoto.

2.1 Kuweka Mbele Maslahi ya Mtoto (Best Interests of Child Standards)

Ibara ya 3(1) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (1989) na Ibara ya 4 ya Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (1990) na kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Mtoto 2009 inatamka kuwa katika utekelezaji wa masuala yoyote yanayomhusu mtoto utakaofanywa na Taasisi za Serikali au watu binafsi; Mahakama au ngazi za utawala ni lazima utekelezaji huu

uzingatie maslahi bora mapana ya mtoto.Hata hivyo sera ya Maendeleo ya Mtoto ya 1996 iliyorekebishwa mwaka 2008 inatambua haki za mtoto kama zilivyoainishwa katika mikataba ya kimataifa na suala la maslahi bora ya mtoto yanatakiwa kupewa kipaumbele.

Mikataba hii miwili inataka hatua zozote zinazochukuliwa na Serikali; Bunge au Mahakama zizingatie kwa kina maslahi mapana ya mtoto kwa kujiuliza ni kwa namna gani maamuzi yatakayotolewa yatakuwa na athari kwa watoto. Hili linapaswa kuzingatiwa hata kama uamuzi huu hauna athari ya moja kwa moja kwa Mtoto.

Jukumu hili linaweza kufanikiwa endapo mambo haya yataingizwa kwenye Katiba inayoandikwa sasa tukitambua kuwa Watoto ni kundi dhaifu katika jamii na linahitaji kuangaliwa kwa mapana yake. Hivyo basi kanuni ya maslahi mapana ya mtoto inatazama mahitaji, matarajio na hisia za mtoto ambavyo ni mambo muhimu wakati wa kusimamia haki za binadamu kwa Watoto.

2.2 Kuepuka na Kuondoa Ubaguzi

Kamati ya Kimataifa ya Haki za Binadamu ilitoa tamko Namba 17 la mwaka 1989 ambalo lilifafanua ubaguzi (discrimination) kuwa ni utaratibu aomnyima mtu haki ya aina fulani kwa sababu ya kukosa kigezo kama vile utaifa, rangi, jinsia, dini, mtazamo wa kisiasa, utaifa wake, jamii anayotokea; mali, uzazi au aina nyinginezo za hadhi ambazo zinazuia kwa namna moja au nyingine kufurahia haki na uhuru wa binadamu. Tamko hili pia lilitambua watoto hawapaswi kubaguliwa kwa sababu yoyote ile.

Vilevile ibara ya 2 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa inaitaka nchi mwanachama *kuheshimu na kuwapatia wananchi wote katika utawala wake haki zote zilizomo katika mkataba huu bila ya kuonyesha ubaguzi wowote wa rangi, utaifa, jinsi, lugha, dini na umri.*

Ibara ya 24 ya Mkataba huu inakwenda mbali zaidi kwa kutamka *kuwa kila mtoto ana haki ya kulindwa na familia yake, jamii yake au taifa lake bila aina yoyote ya ubaguzi unaotokana na rangi, jinsi, lugha; , rangi, , dini, mtazamo wa kisiasa, utaifa wake, jamii anayotokea; mali, uzazi au aina nyingine za hadhi.*

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto pia unatambua kuwa katika nchi mbalimbali wapo watoto wanaoishi katika mazingira magumu na wanahitaji uangalizi maalum. Ibara ya 2 ya Mkataba huu kwa kutambua hili inaitaka nchi mwanachamana *kufanya kila iwezalo kuhakikisha watoto wanalindwa na kuepushwa na aina zote za ubaguzi, mateso na adhabu kutokana na hadhi yao, matendo yao au mawazo yao.* Makatazo haya ya ubaguzi pia yako katika Mikataba ya Kimataifa inayozuia Ubaguzi Dhidi ya Wanawake na ule Unaozuia Ubaguzi wa Rangi.

Kwa kutekeleza majukumu yake yanayotokana na mikataba ya Kimataifa, Tanzania imepiga marufuku kupitia Katiba na sheria mbalimbali aina zote za ubaguzi. Katiba ya sasa ya Tanzania ya mwaka 1977 katika ibara ya 13(5) na 13(6) inakataza *ubaguzi rangi, utaifa, jinsi, lugha;*

utaifa, rangi, jinsia, dini, mtazamo wa kisiasa, utaifa wake, jamii anayotokea; mali, uzazi au aina nyinginezo za hadhi.

Katika kutekeleza masharti ya Katiba, Tanzania imetunga sheria mbalimbali zinazokataza ubaguzi kwa minajili ya kutoa usawa kwa wote ikiwamo Watoto. Ubaguzi wa watu ikiwa ni pamoja na watoto pia unakatazwa na Sera mbalimbali za nchi.

Sera ya Maenedeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 inakataza ubaguzi unaotokana na jinsi au unaotokana na nafasi ya mtoto katika maisha. Sera ya Taifa ya Elimu na Sera ya Taifa ya Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 pia zinakataza ubaguzi. Kwa upande wa Sera ya Wenye Ulemavu inatamka wazi kuwa Tanzania inathamini haki za Watoto na usawa wa binadamu wote na kusisitiza kuwepo kwa sheria inayotoa nafasi kwa raia kushiriki moja kwa moja katika shughuli zinazomjenga yeye na jamii kwa ujumla. Sera pia inatambua kuwa watu wenye ulemavu wana haki sawa ya kupata mahitaji yao muhimu kutoka kwa jamii bila ya kubaguliwa kwa sababu yeyote pamoja na ulemavu wao.

Kifungu cha 7(i) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kinapiga marufuku ubaguzi katika sehemu za kazi. Katika sheria hiyo aina za ubaguzi zimeainishwa kwa uwazi katika kifungu cha 7(4) cha sheria na kinajumuisha makatazo ya ubaguzi kwa misingi ya *rangi, jinsi, lugha;, mtazamo wa kisiasa, utaifa wake, jamii anayotokea; uwezo wa mali, uzazi au aina nyinginezo za hadhi, ujauzito, kusumbuliwa na maradhi ya UKIMWI, umri n.k*

Kifungu cha 31 cha Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008 kinakataza aina yoyote ya unyanyapaa na ubaguzi kwa kigezo cha kuwa na UKIMWI au kuhisiwa kuwa na UKIMWI. Vilevile kifungu cha 29 kinamtaka kila mtoa huduma za afya anayemhudumia mgonjwa mwenye UKIMWI kutoa huduma bila kuwa na aina yoyote ya unyanyapaa na ubaguzi. Katika sheria hii pia Taasisi mbalimbali zinazuiwa kumnyima mtu nafasi ya kujiendeleza au kujiunga na mafunzo au kumfukuza mtu kazi kwa kigezo cha hali ya afya yake kwa kuhisiwa au kuonekana kuwa ana UKIMWI. Kunyanyapaa pia kunakatazwa kutumiwa kama kigezo cha kumzuia mtu kusafiri; kupata kazi au kuishi sehemu mbalimbali katika nchi au nje ya nchi. Sheria imeweka pia makosa ya kijinai kwa mtu anayekiuka masharti ya kuzuia unyanyapaa kwa kuweka faini isiyozidi milioni mbili au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja.

Sheria ya Ulemavu iliyopitishwa na Bunge mwezi Aprili mwaka, 2010 inaipa Sera ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004 nguvu ya kisheria pamoja na kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Watu wenye Ulemavu. Sheria hii inawapatia watu wenye ulemavu haki za kupata huduma za kijamii kama vile afya, elimu, ufundi stadi na ustawi wa jamii. Vilevile inawapatia haki za kupata ajira; kufika sehemu mbalimbali bila ya vikwazo na haki ya mawasiliano. Sheria hii pia inakataza aina zote za ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu. ia inampa Waziri mwenye dhamana ya ustawi wa jamii wajibu wa kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata huduma stahiki bila ya ubaguzi. Ili kuhakikisha dhana hii ya kutowabagua wenye ulemavu inatiliwa mkazo Kifungu cha 6 cha sheria ya watu wenye ulemavu inaitaka serikali kufanya kila iwezalo kuhakikisha walemavu wanapata haki ya usawa kwa kupiga marufuku aina zote za unyanyapaa na kuweka mfumo wa sheria unaojali na kustawisha haki za wenye ulemavu kwa kukataza ubaguzi.

Katika kifungu cha 5(1) cha sheria ya Mtoto, mtoto amepewa haki ya kuishi bila kubaguliwa kwa sababu ya jinsia; kabila; umri; dini; lugha; mtazamo wa kisiasa; ulemavu; hali ya afya; mila; mahali atokako; hali ya uchumi na kijamii; hali ya kuwa mkimbizi au hali nyingine yoyote.

Kwa mifano tuliyoorodhesha hapo juu, ni dhahiri kuwa kunahitajika ibara mahususi ya Katiba inayopiga marufuku ubaguzi kwa watoto. Baadhi ya nchi zilizoipa mkazo haki hii ni pamoja na Afrika Kusini na Uganda.

2.3 Kushirikisha Watoto na Haki ya Kusikilizwa na Kuheshimu Mtazamo wa Mtoto)

2.3.1 Umuhimu wa Haki ya Mtoto ya Kusikilizwa.

Haki ya kusikilizwa iliyoko katika ibara ya 12 ya Mkataba wa CRC inatambuliwa kama haki ya msingi inayotegemewa katika utekelezaji wa haki zingine zote. Ibara ya 12 inaweka msisitizo kuwa watoto wana uwezo wa kutoa mawazo yao na hivyo wanapaswa kupewa haki ya kusikilizwa. Haki hii inapaswa kutolewa kwa watoto wa kike na kiume bila kujali umri wao; watoto walioko mijini na vijijini; watoto walioko katika makabila madogo na watoto wenye ulemavu.

Katika mazingira ya Tanzania utekelezaji wa Ibara ya 12 ya CRC inatupasa kufanya yafuatayo:

- Kuanza kusikiliza kwa makini Watoto wanataka nini
- Kutambua kuwa mawazo yanayotolewa na Watoto yanatokana na mazingira wanayokutana nayo katika maisha ya kila siku
- Kuanza kuhoji wajibu wa watu wazima katika kuhudumia Watoto.

Hata hivyo, kwa kutambua kuwa Watoto wana haki hakuondoi wajibu wa watu wazima kwa Watoto bali kunaongeza chachu ya watu wazima kushirikiana na Watoto kupigania haki za Watoto. Kinachosisitizwa na CRC ni kwa watu wazima kutambua kuwa wanapaswa kufanya kazi na Watoto kwa karibu sana ili kwa pamoja waweke mikakati ya kuleta mabadiliko na kudai haki zao.

Kwanini watoto wanataka kushiriki katika kuunda Katiba mpya

- Watoto wana mambo yanayowahusu ambayo yanapaswa kuingizwa katika Katiba mpya
- Watoto wanahisi wakati mwingine watu wazima wanapozungumzia mahitaji yao hawaelezi kile wanachopaswa kukisema au wanapokisema hukikosea.
- Watoto wanadhani ni sahihi kusikilizwa hasa kwa mambo yanayoathiri maisha yao
- Watoto wanadhani mchango watakaoutoa wao utaleta msukumo na changamoto zaidi kuliko utakaposemewa na watu wazima
- Watoto wanataka kushiriki ili kuifanya Tanzania iwe ni mahali pazuri kwa wao kuishi kwa kuwa wanatarajia kuishi muda mrefu zaidi kuliko watu wazima
- Kushiriki katika mchakato kunawajenga na kuwaimarisha kiakili
- Ni nafasi ya wao kukutana na Watoto wenzao kutoka katika mazingira tofauti; umri tofauti na waliopitia uzoefu tofauti.

Kushiriki katika maamuzi ni haki ya msingi ya binadamu na mhimili mkuu wa kutazama haki za Watoto kama haki za binadamu. Kushiriki kunaashiria ushiriki wa wadau wa haki hizo kuzidai

na kuhoji watendaji juu ya utekelezaji wake. Ushiriki wa wadau na kuwahoji watendaji huunda mfumo sahihi wa kutazama haki za Watoto kama haki za binadamu.

Katika kusisitiza uandikaji wa ibara itakayojadili haki za Watoto kutoa mawazo yao, ni muhimu kufahamu nini ibara ya 12 ya CRC inatamka na nini isichotamka.

- Haitoi mwanya wa Watoto kujiamulia mambo yao wenyewe. .
- Haiwapi Watoto haki ya kutoa maamuzi yanayowahusu bila ya kuangalia athari ya maamuzi hayo kwao wenyewe au kwa wenzao.
- Haiwapi Watoto uwezo wa kutojali haki za wazazi kwa watoto wao.
- Hata hivyo ibara hii inaingiza aina mpya ya changamoto inayoleta hojaji kwa mawazo mgando ya kizamani yanafikiri kuwa watoto wanapaswa kutazamwa tu na sio kusikilizwa.

2.3.2 Haki ya Mtoto Kushirikishwa Inahusisha nini?

Ibara ya 12 ya CRC, inajumuisha mambo yafuatayo:

- Watoto wote wana uwezo wa kutoa mawazo
- Watoto wana haki ya kutoa mawazo yao kwa uhuru bila kushurutishwa
- Watoto wana haki ya kusikilizwa katika maswala yote yanayowahusu
- Watoto wana haki ya kutaka mawazo yapewe msisitizo unaostahili
- Watoto wana haki ya kushiriki katika shughuli mbalimbali zinazolingana na umri wao au kupevuka kwao.

Haki hizi zimeelezewa kinagaubaga kama ifuatavyo:

- **Watoto wana uwezo wa kutoa mawazo:** Hii inamaanisha kuwa hakuna umri wa chini unaozuia mtoto kushirikishwa. Hivyo hii ni haki inayogusa mtoto yeyote mwenye hoja ya kujadili. Haki hii pia inawagusa hata watoto wadogo (ikiwa ni pamoja na wenye ulemavu) ambao wanapata shida ya kujieleza kwa ufasaha na inashauriwa hawa wapewe nafasi ya kujieleza kwa njia mbadala za mawasiliano kama michoro, ushairi, maigizo, maandishi, kwa kutumia kompyuta au kwa lugha ya alama.

- **Watoto wana haki ya kutoa mawazo yao kwa uhuru bila kushurutishwa:** Hii inamaanisha kuwa kama nafasi imejitokeza ni wajibu wa watu wazima kuwatengea Watoto nafasi. Wajibu huu umewekwa katika ibara ya 12 ya CRC kwa watu wazima kwa nafasi yao kama wazazi; wataalamu na wanasiasa kuhakikisha kuwa watoto wanawezeshwa na kupewa hamasa ya kuchangia mawazo kwenye masuala yote ya muhimu. Hata hivyo hii haimaniishi kuwa ni lazima Watoto watoe maoni hata pale ambapo hawana nia wala ulazima wa kuchangia.

- **Watoto wana haki ya kusikilzwa katika masuala yote yanayowagusa:** Hii inaamanisha kuwa watoto wanapaswa kushiriki kutoa mawazo katika masuala yote yanayogusa maisha yao kama masuala ya familia; shule; katika mitaa na vijiji wanavyoishi na hata katika masuala ya kitaifa. Haki hii inapaswa kutumiwa kwa masuala yote yanawagusa mtoto mmoja mmoja; kwa mfano ni wapi Watoto wanapaswa kuishi baada ya wazazi kutalikiana, au masuala yanayogusa watoto kwa ujumla wao kama vile kutungwa kwa sheria inayoweka masharti ya umri wa mtoto kuajiriwa. Ni vizuri

kutambua kuwa maeneo mengi ya utekelezaji wa sera na sheria zenye maono ya maendeleo ya kijamii kwa mfano hoja zinazogusa usafiri; makazi; sera za kiuchumi; mazingira; elimu; afya ya mtoto na afya ya jamii yanamgusa mtoto moja kwa moja.

- **Watoto wana haki ya mawazo yao kutiliwa mkazo:** Hii inamaanisha kuwa watoto si tu wana haki ya kutoa mawazo bali pia mawazo yao kupokelewa kwa uzito unaostahili. Ibara ya 12 ya CRC inatamka bayana kuwa mawazo ya watoto yapewe uzito unaonstahili na uamuzi unaotolewa uwe unawahusu. Hata hivyo hii haimaanishi kuwa ni lazima kila wazo la mtoto ni lazima lifuatwe. Kinachotakiwa ni kuyazingatia mawazo hayo.

- **Watoto wana haki ya kushirikishwa kulingana na umri na kupevuka kwao:** Hii inamaanisha kuwa uzito wa jambo linaloelezwa na mtoto ni lazima lilinganishwe na umri wa mtoa hoja. Hii haimaanishi kuwa mawazo ya watoto hayatapewa uzito na kipaumbele. Yapo mambo ambayo watoto wadogo wanaweza kuyaelewa na kuyatolea hoja. Umahiri si jambo linaloweza kuletwa ndani ya muda mfupi. Ni lazima kuzingatia mazingira ya kijamii; uamuzi unaopaswa kutolewa; mazingira halisi ya changamoto alizopitia mtoto huyu na msaada aliopatiwa na watu wazima vinaweza kuathiri namna mtoto anavyoelewa jambo linalomzunguka.

2.3.3 Umuhimu wa kumpatia mtoto haki ya kushiriki

Athari ya Ibara ya 12 inaweza kuonekana katika haya yafuatayo: Ni haki ya msingi, inayompa mtoto nafasi ya kuwa nyota wa maisha yake na kuwa mshiriki katika maamuzi yatakayomuathiri. Hata hivyo ni vizuri pia kufahamu kuwa kama ilivyo kwa watu wazima; ushiriki wa kidemokrasia pekee hautoshelezi ila ni njia muafaka ya kutoa haki; kuchochea mabadiliko na kutambua wanaotumia madaraka yao vibaya. Vilevile tunaweza tukasema hizi pia ni haki za kitaratibu zinazowawezesha watoto kupinga unyanyasaji au kutelekezwa na kuvunjwa kwa haki zao; na kuchukua mamlaka ya kuboresha haki hizi. Inawawezesha Watoto kushiriki, kuchangia na kudumisha maslahi yao kwa upana.

2.3.4 Athari ya kutomsikiliza mtoto na kutozipa umuhimu hoja wanazotoa

Upo ushahidi wa kutosha na wa wazi kuonyesha kwamba mtazamo wa jamii kwa watoto unaochagizwa na imani kuwa wazazi ndio wanajua kwa undani mahitaji ya watoto na maslahi yao, umeshindwa. Makosa haya kwa kiasi kikubwa yanajionyesha pale watoto wanaponyimwa haki ya kusikilizwa. Baadhi ya mifano hii ni:-

- **Watoto kudhalilishwa na watu wanaowazidi umri:** Uzoefu unaonyesha kuwa pale ambapo watoto wamenyimwa nafasi ya kushiriki katika maamuzi kuhusu mambo yanayowahusu au pale ambapo mawazo yao hayakupewa kipaumbele stahiki, watu wazima walichukua maamuzi yanayowagusa Watoto na kusababisha Watoto kunyanyaswa na kudhalilishwa na hivyo kuwaathiri.

- **Si wakati wote wazazi wanaweka mbele maslahi ya Watoto:** Uzoefu uliokusanywa karne iliyopita umeonyesha kuwa watu wazima hasa wasomi wanaojihusisha na masuala au wenye majukumu yenye kuhusiana na Watoto wamekuwa ni chanzo cha kutoa uamuzi, sera na mikakati isiyofaa au ile inayomdhuru mtoto huku wakidai kuwa wana lengo la kusimamia ustawi wa Watoto.

- **Haki za wazazi hupewa uzito zaidi ya zile za Watoto:** Mara nyingi Taratibu mbalimbali za kijamiii zimekuwa zikitoa mkazo zaidi kwa haki za wazazi hata pale inapoonekana kuwa athari za upendeleo huu zina madhara zaidi kwa ustawi wa Watoto. Hii inatokana ukweli kwamba wazazi kama watu wazima na wenye haki ya kupiga kura , wanao uwezo mkubwa wa kushawishi kwa kuwa kwa kupitia sanduku la kura waweza kuamua ni nani awe katika ngazi za utawala[3]. Watoto kwa bahati mbaya hawana haki ya kushiriki katika kupiga kura kwa mustakabali wa kiutawala au kitaifa.Hii itajidhihirisha hata katika hatua mbali mbali za mchakato huu wa kuwa na Katiba Mpya.

- **Maslahi ya Watoto mara nyingi hayapewi msukumo kwenye sera za kitaifa:** Maslahi ya Watoto katika sera za kitaifa mara nyingi hayapati msukumo unaostahiki kwa kuwa ni kundi dhaifu ukilinganisha na Makundi mengine. Hii haimaanishi kuwa maslahi haya huachwa kwa makusudi bali inamaanisha kuwa sauti za Watoto na athari za sera na mipanago kwa maslahi ya Watoto hayaonekani kwenye macho ya watendanji wenye kutoa uamuzi na kwa sababu hiyo hayawezi kuwa ajenda muhimu katika ngazi za kisiasa.

2.3.5 Faida ya Kuwasikiliza Watoto na Kupokea Mawazo na Hoja zao

Uzoefu kutoka katika jamii mbalimbali unaonyesha kuwa endapo Watoto watashiriki katika kutoa uamuzi au mipango inayowahusu au kuwaathiri na mawazo hayo yakapewa uzito unaostahili, haki za watoto na ustawi wao zitalindwa na kuimarishwa. Yafuatayo ni matokeo chanya yanayoweza kutokea endapo Watoto watasikilizwa na hoja zao kutiliwa maanani:

- **Huchochea maamuzi bora:** Watoto wana ufahamu na uzoefu wa kutosha katika masuala yanayowahusu na wanaweza kutoa mawazo bora kutokana na uzoefu huo. Pamoja na ukweli kuwa sera nyingi za serikali zina athari ya moja kwa moja au athari isiyo dhahiri kwa watoto, bado sera hizo zimeendelea kutungwa na kutekelezwa bila kujali ni kwa jinsi gani zinaathiri maisha ya kila siku ya Watoto katika wakati wa sasa na baadaye.

- **Inaimarisha na kuboresha ufahamu na utekelezaji wa dhana ya demokrasia:** Ni dhahiri kuwa katika nchi zetu ambazo demokrasia inakua na hata katika zile nchi ambapo demokrasia imepanuka Watoto wanapaswa kupata uzoefu wa maamuzi yanayofanywa kidemokrasia. Watoto wanahitaji kufahamu kuhusu haki zao na wajibu wao na namna haki zao zinavyodhibitiwa na haki na wajibu wa wengine. Watoto wanahitaji nafasi ya kushiriki katika kufanya maamuzi kupitia shuleni na katika jamii zao na kuheshimu makubaliano yatakayofikiwa. Ushiriki wa namna hii huwafanya Watoto kujenga tabia bora itakayowafanya wawe raia wema wakiwa watu wazima.

[3] Kwa mfano, adhabu zinazodhuru mwili wa mtoto zimekuwa zikitolewa katika nchi nyingi duniani licha ya Kamati ya Kimataifa Haki za Watoto (CRC) kutamka bayana kuwa adhabu hizo zinapingana na matakwa ya Ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto inayotaka Watoto kupewa ulinzi dhidi ya aina yoyote ya unyanyasaji wa kutumia nguvu. Wazazi wameendelea kuitumia aina hii ya adhabu kwa madai kuwa ni muhimu katika kuleta nidhamu kwa Watoto wao.

- **Inawalinda watoto zaidi:** Tunajifunza kuwa tuna haki na kuanza kuziamini kupitia hatua ya kutenda. Kuwa na sauti kuhusu haki zako ni nguzo muhimu katika kuifuatilia haki yako. Ni dhahiri kuwa pale ambapo Watoto wamepewa nafasi ya kudai haki zao, unyanyasaji na uvunjaji wa haki ulibainika kwa urahisi zaidi. Watoto wanaopewa nafasi ya kuongelea haki zao pia hujengewa uwezo wa kuzidai pale zinapokiukwa na mara nyingi wanaweza kuzidai bila ya kuwategemea watu wazima.

- **Ni haki ya binadamu:** Katika mtazamo wa haki za binadamu kila binadamu ana haki ya kutoa maoni kuhusu uamuzi unaoweza kuathiri maisha yao. Haki hii ni kwa kila mtu hata kama ni mtoto.

a. Kanuni zinazoongoza mchakato wa ushiriki wa watoto

Katika maisha ya kila siku zipo kanuni za msingi zenye kutoa mwongozo wa namna Watoto wanavyoweza kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kushiriki katika masuala mbambali. Baadhi ya kanuni hizo za msingi ni:

- Watoto kutambua lengo la mchakato ulio mbele yao, malengo yao na nafasi yao katika mchakato huo.
- Kuwepo kwa Uwazi wa namna uamuzi utatolewa na nani atatoa uamuzi
- Watoto washirikishwe kuanzia mwanzo wa mchakato wa uamuzi
- Watoto wasibaguliwe kwa kutumia vigezo vya aina yeyote ikiwemo vigezo vya umri, hali yao; kabila au uwezo.
- Watoto lazima waelezwe mapema kanuni na taratibu za msingi zitakazofuatwa
- Ushiriki uwe ni kwa hiari ya mtoto na mtoto apewe nafasi ya kujiondoa katika ushiriki wakati wowote anapoona inafaa
- Mawazo ya Watoto yanapaswa kuheshimiwa na kuzingatiwa

i. Kuwahudumia Watoto na kuwapa ulinzi

Kwa mujibu wa taratibu za kimataifa kama zilivyoainishwa katika Mikataba mbalimbali serikali zina wajibu wa kuwalinda raia wake na kuwapatia huduma mbalimbali za msingi. Serikali ya Tanzania pamoja na kulitambua jukumu hili imejaribu kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na za kisheria kulikwepa jukumu hili. Hali hii inajionyesha wazi kwa namna ilivyozuia kupatikana kwa haki za Binadamu zilizoainishwa kwenye Katiba kwa kutumia mbinu ya kuweka vifungu vinavyyominya haki kwa mlango wa nyuma na hivyo kuifanya haki iliyotolewa kukosa wigo wa kutekelezeka. Aina hii ya uminywaji wa haki inajadiliwa sana na wasomi wa sheria na wanazuoni. Mfano wa karibuni ni kitendo cha serikali kukataa kuingiza kipengele wakati wa utungaji wa sheria ya mtoto kinachoaininsha wajibu wa serikali.

TCRF na Asasi zingine za kiraia zinapendekeza kuingizwa katika Katiba tamko mahususi kuhusu wajibu na jukumu la serikali katika kustawisha, kulinda, kutimiza, kuwezesha kushamiri kwa haki za Watoto na haki za binadamu kwa ujumla.

3. 0 HAKI MAHSUSI ZA WATOTO ZINAZOPASWA KUZINGATIWA KATIKA KATIBA MPYA

Katika sehemu hii, TCRF inatoa mapendekezo kuhusu haki za muhimu zinazopaswa kuingizwa kwenye Katiba ili kuweka msingi wa kuheshimu na kulinda haki za Watoto. Haki hizi zinazoorodheshwa hapa sio kwamba ndio pekee zinatakiwa kwenye Katiba bali ni haki za msingi ambazo kwayo haki nyingine nyingi za kiKatiba hupatikana. Vilevile haki hizi zinatoa msingi wa namna sheria nyingine za nchi zinavyopaswa kutungwa ili kuendana na misingi na masharti ya Katiba. Baadhi ya haki zilizoorodheshwa hapa ni pamoja na haki ya kuwa na jina na utambulisho; haki ya elimu; afya; haki ya kushiriki; haki ya kulindwa hasa pale mtoto anapoingia katika mikono ya sheria na nyinginezo, Mapendekezo haya yanawakilisha zile haki za msingi ambazo zinajenga msingi wa haki zingine.

3.1 Haki ya kuwa na Utambulisho (kuwa na Jina, Utambulisho wa Utaifa na kuwatambua)

Wajibu wa kwanza wa serikali kwa mtoto unaanzia pale mtoto anapozaliwa na kuandikishwa katika orodha ya vizazi. Kitendo hiki cha kumuandikisha mtoto huashiria kuwa seriakli imemtambua uwepo wa mtoto huyu na umuhimu wake na hujenga msingi wa namna haki zake za baadaye zitakavyolindwa.

Haki hii ni moja ya haki zinazotambuliwa zaidi katika mikataba mingi ya Kimataifa kama vile Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu, CRC na ACRWC.

Mijadala mingi katika kuingalia haki hii imejikita zaidi katika kutazama ni kwa namna gani uandikishaji unaweza kufanyika bure na kuwahusisha watu wote na namna gani haki hii ya kuandikishwa, au kusajiliwa kwa maneno mengine, inaweza kuhusishwa na utaifa au uraia. Hivyo wakati wote haki hii hutafsiriwa namna ambavyo serikali inatimiza majukumu yake katika kulinda haki za kiraia, kijamii, kitamaduni na haki za kiuchumi za watu wake na namna watu wanaweza kuzidai haki hizi.

CRC katika moja ya maoni yake imewahi kuelezea kuwa kushindwa kuwaandikisha Watoto wanapozaliwa ni ushahidi tosha kuwa serikali haitaki kuwatambua Watoto kama kundi maalumu la watu mbele ya sheria na hivyo kuzorotesha namna kundi hili linavyoweza kufurahia haki zao za msingi.

Vilevile kamati ya Kimataifa ya Haki za Binadamu katika tamko lake kuhusiana na ibara ya 24 ya ICCPR ilihusisha umuhimu wa kuwaandikisha Watoto kama njia maalumu ya kumpa mtoto haki yake kama binadamu. Mtazamo huu pia ulikubaliwa na ripoti ya timu ya wataalamu waliokutana kujadili namna sheria zinavyoweza kutumika kuwasaidia masikini, iliyotambua haki ya kuandikishwa baada ya kuzaliwa kama mojawapo ya nyenzo muhimu ya kisheria ya kulinda haki za kiuchumi za wananchi, haswa katika suala zima la kufikia mifumo rasmi kama vile hifadhi ya kijamii na umiliki mali.

Katika mtazamo wa jumla, inapedekezwa kuwa kila taifa lihakikishe kuwa uandikishaji wa vizazi unakuwa wa bure, wa lazima na uwahusu watu wote. Kwa kuwa bure inamaanisha kuwa dola inabeba jukumu la kutengeneza mfumo ambapo uandikishaji unafanyika kwa ufanisi na dola

inafaidika kwa kuweza kupanga mipango yake ya namna ya kutoa huduma kwa watu wake kama vile huduma za chanjo; afya na elimu. Lengo hasa likiwa ni kuhakikisha kuwa uandikishaji unakuwa sehemu ya mipango ya Maendeleo.

Inapendekezwa pia uandikishwaji uwaguse Watoto wote walioko ndani ya dola husikia bila ya kujali wana uraia wa nchi gani. Lengo la kuweka sharti hili ni kuhakikisha Watoto wanatambulika na kuonekana hasa kutokana na baadhi ya dola kuweka sheria na taratibu zinazozuia watu wenye asili fulani kupata huduma za msingi kutoka nchi husika. Vitendo hivi si kwamba havitendeki bali vinatendeka. Kwa mfano CRC imeshawahi kuelezea hali hii wakati ilipokuwa inaangalia taarifa ya Jamhuri ya Dominika baada ya kuwepo tuhuma kuwa serikali yake imeweka vikwazo kwa Watoto wenye asili ya Haiti kuandikishwa shule na kupata huduma za afya kwa kigezo kuwa hawajaandikishwa.

Vilevile katika tamko lake la hivi Karibuni Kamati ya Afrika ya Wataalamu Kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto inayosimamia utekelezwaji wa Mkataba wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACERWC) ilitamka kuwa Kenya imefanya makosa ya kukiuka mkataba wa Afrika wa haki za Watoto na mikataba mingine ya Kimatafia kwa kuzuia uandikishaji watoto wenye asili ya Kinubi. Katika tamko hilo kamati ya ACERWC ilijadili kwa kirefu umuhimu wa kuwa na ibara ya Katiba inayolinda haki ya kuandikishwa. Kwa kutambua hilo ACRWC katika ibara ya 6 inasisitiza sana haki ya mtoto kuwa na jina na haki ya kuandikishwa kuzaliwa kama haki za msingi zinazoendana na haki ya kuwa na utaifa na imekuwa ikisisitiza kila taifa kuiweka haki hii katika Katiba zao. Kwa Watoto, haki hizi za kuandikishwa na kuwa na jina zinalandana na haki ya mtoto ya kuwafahamu na kutunzwa na wazazi wake na pale inaposhindikana kuwepo kwa mfumo wa malezi mbadala ya huo. Katiba za Rwanda na Uganda zimeliwekea msisitizo sana jambo hili.

Hivyo ni muhimu pia wakati wa kujadili kuangalia namna familia kama msingi mkuu wa jamii inaweza kulindwa na Katiba,na ni matarajio yetu kuwa hili litakuwa limetolewa kama pendekezo mahususi katika mapendekezo ya makundi mengine, la sivyo, tunakaribisha fursa ya Tume kulitolea ufafanuzi pia kupitia TCRF.
Katiba yetu ya sasa haitambui haki hizi katika tamko lake la haki za binadamu na hivyo kukosa dira ya namna haki hizi zinavyopaswa kulindwa. Sheria ya Sasa ya Uandikishaji wa Vizazi na Vifo (Sura Namba 108) imetungwa ikifuata mfumo wa kikoloni ambao haukuona umuhimu wa kuwasajili wazawa. Vilevile mfumo wa uandikishaji sio mfumo rafiki kwa kuwa sio rahisi kupatikana vijijini kwa kuwa vituo vya uandikishaji vinapatikana ngazi ya wilaya.

TCRF inaamini kuwa endapo Katiba mpya itatambua haki ya kuandikishwa na haki nyingine zinazoambatana nazo, kutakuwa na mabadiliko makubwa yenye manufaa kwa kuchochea mjadala kuhusiana na namna Watoto wanavyopaswa kulindwa na jamii yao. Mfano wa Kenya kuhusiana na namna ilivyolishughulikia tatizo la Watoto wenye asili ya Kinubi ni ushahidi tosha wa umuhimu huu hasa baada ya kutatua tatizo kwa kuingiza suala la uandikishaji katika Katiba ya Kenya. Brazil na Uganda nao pia walifanya hivyo hivyo.

3.2 Haki ya Afya na Haki ya Kuishi

Ni muhimu kutambua kuwa ipo mifano mingi ya nchi zilizopitia aina za michakato ya Katiba kama wetu na zikafanikiwa kuingiza haki hizi katika Katiba zao. Baadhi ya nchi hizo ni Afrika Kusini; Uganda na Kenya. Hivyo ni jambo la kutia moyo endapo Tanzania itafuata nyayo za nchi jirani ambazo zote zinaunda Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Katiba yetu ya sasa inatambua katika Tamko lake la Haki za Bindamu haki ya afya, elimu, haki ya kuishi, kutoa mawazo, haki ya kushiriki katika shughuli mbalimbali na haki ya kutokubaguliwa. Hata hivyo haki hizi si kwa Watoto pekee bali na watu wazima. Ibara ya 14 inatoa haki ya kuishi kwa watu wazima na Watoto.

Haki ya afya ni haki jumuishi inayohusisha haki na mahitaji (entitlements) na hupaswa kutolewa bila ya ubaguzi. Ni muhimu pia kutambua kuwa tunapozungumzia kutokuwepo na ubaguzi haimaaishi tu kuwa kila mtu afanywe kuwa sawa na mwingine bali pia kunamaanisha kutambua haki za kila mmoja na za Makundi hasa Makundi maalum ya wanyonge. Vilevile ni muhimu kutofautisha haki ya afya na haki ya kuwa mwenye afya. Inamaanisha kuwepo kwa usawa katika kupata huduma za afya zinazomwezesha mtu kuwa na afya njema.

Pamoja na ukweli kwamba watoto na vijana wanajumuishwa pamoja ni kundi lenye mahitaji yanayotofautiana kulingana na umri, ukomavu; mazigira na tamaduni za sehemu husika . Itakumbukwa kwamba mtoto katika CRC ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18. Upendeleo maalumu unapaswa kutolewa kwa vijana wa umri wa miaka 15 – 18 kwa sababu kundi hili mara nyingi huwa ni kundi lililosahaulika ingawa kuna ushahidi kuwa ni kundi nyonge.

Haki ya afya ni lazima ifurahiwe na watu wote bila ya kubaguliwa kwa vigezo vya jinsi; umri; hali ya kiuchumi na kijamii; ulemavu; mahali mtu atokapo; au hali yake ya ukimbizi ikiwa ni pamoja na hadhi ya mzazi au mlezi. Afya lazima itafsiriwe kuwa inahusisha zaidi maumbile ya mwili kwa kujumuisha afya ya akili na ya kiroho.

Mfumo wa sasa wa sheria ya afya ya jamii kama ulivyoainishwa katika Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 unaitaka serikali kuiboresha, kudumisha na kuimarisha sekta ya afya ya Jamii kwa kuhakikisha utolewaji wa huduma kamili na endelevu za jamii kwa raia wote. Sheria hii inamtazama mtoto kama mtu mwenye umri chini ya 18. Kifungu cha 19(1) kinaangalia umuhimu wa kutoa kinga dhidi ya magonjwa kwa mama na mtoto.

Sheria ya watu wenye ulemavu namba 9 ya mwaka 2010 inatoa mwongozo wa namna ya kutoa huduma za afya; ustawi wa jamii; elimu na mafunzo ya Ufundi; ajira na kulinda haki za binadamu kwa watu wenye ulemavu.

Kwa kutumia kigezo hiki ni wazi kuwa usawa katika kupata huduma za kiafya na haki ya kuishi havijashughulikiwa kwa ukamilifu katika sheria zilizopo. Katiba inayotungwa ina jukumu la kuhakikisha kunakuwepo na sheria bora zitakazotoa miongozo ya namna haki hizi zitaimarishwa.

3.3 Haki ya Kupata Elimu

Ibara ya 26 ya Tamko la Haki za Binadamu la Mwaka 1948 linampa kila mtu haki ya kupata elimu ikiwa ni pamoja na elimu bure ya msingi. Tamko hili likaongezwa uzito na ibara ya 13(1) ya ICCPR inayotaka kuwepo kwa elimu ya bure ya msingi. Msisitizo kama huo pia unatolewa na CRC katika ibara ya 28 na ACRWC katika ibara ya 11(11)(a). Pamoja na matamko hayo Umoja wa Mataifa katika Mkakati unaojulikana kama Mkakati wa Dakar wa mwaka 2000 umejiwekea malengo ya kupanua na kuendeleza mpango madhubuti wa elimu ya awali kwa watoto hasa wale waishio katika mazingira magumu au wale walioikosa. Ikumbukwe pia kuwa lengo namba 2 ya Malengo ya Milenia inahusiana na haki hii, na Tanzania ni miongoni mwa nchi za Kusini mwa Afrika zinazofanya vizuri.

Katika Tanzania haki hii ya elimu imetambuliwa na Katiba ibara ya 11(2) ingawa ikiwa na masharti ya uwezo. Ingawa haki ya kupata elimu ipo haiweki wazi jukumu la serikali katika kutimiza upataikanaji haki hii.

Uwepo wa sera na mfumo imara wa kisheria unaosimamia elimu kama vile sera ya elimu, MKUKUTA, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 1995, Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, Sheria ya mtoto ya mwaka 2009 chini ya kifungu namba 9 na nyingine nyingi vimechangia kwa kiasi kikubwa kuiwezesha Tanzania kupiga hatua kubwa kufikia lengo la 2 la Milenia mpaka ifikapo mwaka 2015. Hata hivyo bado kuna mambo yanayohitaji kufanyiwa kazi zaidi hasa mambo yanayohusiana na maslahi ya walimu; upatikanaji wa elimu na ubora wa elimu inayotolewa ili mafanikio haya makubwa yaliyopatikana yasipotee.

Hivyo ni muhimu kuhakikisha kuwa haki hii ya elimu inaimarishwa katika Katiba mpya kwa kuwa inatazamwa kama msingi mkuu wa kufikia Maendeleo.

Kwa kutazama Katiba za wenzetu tunatambua kuwa nchi hizi zimeamua kuiangalia haki ya elimu kwa ujumla wake. Katika nchi kama Afrika Kusini, Kenya na Uganda haki hii imefanywa kuwa haki ya msingi na ya lazima tofauti na Tanzania ambapo bado ni haki ya hiari.

Mfumo wa elimu uzingatie kuimarisha usawa, ubora na ulinganifu wa mahitaji ya kielimu katika ngazi zote ili kuondoa kuondoa matabaka katika jamii. Mfumo ulenge kuandaa mitaala inayoimarisha utaifa kwa kuzingatia upatikanaji kwa watoto wote bila tofauti ili kuandaa watoto wataakao wajiobika kwa jamii na taifa.
Kiwango cha ubora wa elimu kimekuwa kikishuka kwa sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya mara kwa mara na udhaifu wa mitaala na uwekezaji finyu katika sekta ya elimu hususani katika taasisi za umma.
Ubora wa elimu utasaidia kuimarisha uzalendo na kuwa na taifa lenye watoto wanaojitambua.

3.4 Haki ya Kutoa Maoni

Ibara ya 19 ya Tamko la Haki za Binadamu la Mwaka 1948 (UDHR) inatamka kuwa kila mtu anayo haki ya kutoa maoni na kujieleza bila ya kizuizi. Pia inajumuisha haki ya kutafuta na kutoa Habari na mawazo kupitia njia mbalimbali bila kujali mipaka.

Ibara ya 12 ya CRC inazitaka nchi wananchama kuhakikisha kuwa Watoto wenye uwezo wa kutengeneza hoja au maoni wanapatiwa fursa hiyo ya kutoa maoni katika mambo yanayowagusa. CRC pia inataka maoni hayo ya Watoto yapewe uzito unaostahili kulingana na umri na upevu wa mtoto husika. Kwa msingi huo CRC inataka mtoto apewe fursa maalum ya kusikilizwa katika mahakama au mabaraza ya kiutawala aidha kwa kupitia yeye mwenyewe; mwakilishi wake au chombo kingine chenye mamlaka katika maamuzi yanayomuathiri moja kwa moja kulingana na taratibu na sheria za nchi husika.

Ibara ya 7 ya mkataba wa ACRWC inatamka kuwa mtoto yeyote mwenye uwezo wa kutoa maoni ana uhuru wa kutoa maoni hayo bila hofu huku akizingatia makatazo yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa nchi ya Tanzania haki hii ya kutoa maoni inapatikana katika ibara ya 18 ya Katiba ingawa haki hii haikulengwa kwa mtoto pekee bali ni haki ya kila mtu. Hata hivyo haki hii imeongezewa nguvu na kifungu cha 11 cha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inayotoa uhuru kwa mtoto kutoa maoni na inakataza mtu yeyote kumzuia mtoto kutoa maoni katika masuala yanayomhusu yeye na ustawi wake.

Watoto wana ujuzi na ufahamu wa mambo yanayowahusu kuliko tunavyowadhania. Ufahamu huu unatokana na namna wanavyohusiana na mazingira yao kwa hiyo ni muhimu sana kuzingatia maoni yao. Ni muhimu pia kufahamu kuwa kutoa maoni hakumaanishi kuwa lazima maoni ya mtoto yazingatiwe. Kinachotakiwa ni kwamba maoni ya mtoto yapewe uzito unaostahili na yapimwe katika mizania sahihi. Ni vizuri kwa watoto kupewa nafasi ya kutoa mawazo na kuchukua majukumu yatakayomjenga na kumuimarisha katika mtazamo wake na kumfundisha kuheshimu maamuzi ya kidemokrasia. Katika mchakato huu ni wajibu wa wazazi na watu wazima kutoa muongozo wa nini kifanyike huku wakizingatia umri na kupevuka kwa mtoto. Hii itasaidia kuondokana na dhana ya kizamani kuwa mzazi anajua mahitaji ya mtoto wake na hivyo mtoto hapaswi kuelezea mahitaji yake.

Mipangilio madhubuti na endelevu ya kukuza ushiriki wa watoto huleta matokeo mazuri kwa mtoto na jamii inayomzunguka. Kama ushiriki wa watoto utahimizwa na utafanywa kwa manufaa ya jamii nzima ni dhahiri kuwa itambadilisha mtoto; itaongeza ulinzi na itahamasisha utunzi wa sera bora zinazozingatia utawala bora na kuwajibika.

Kutokana na kushiriki kwao katika mchakato na kufanya maamuzi, watoto hupata uzoefu; hujenga kujiamini na kujitambua. Hivyo TCRF inaamini ushiriki wa watoto katika mchakato wa uundaji wa Katiba ya Tanzania hujenga uzalendo na humfanya mshiriki kujihisi na yeye ni sehemu ya chachu ya mabadiliko.

3.5 Haki ya kuwa na Mfumo Rafiki wa Haki kwa Watoto walio katika Ukinzani na Sheria

Mfumo rafiki wa sheria za kijinai kwa watoto ni kipimo sahihi cha namna serikali inavyoweza kutekeleza matakwa mbalimbali ya mikataba ya kimataifa na sheria na sera za watoto. Tuna nafasi ya pekee ya kufanya mabadiliko na kufanya mfumo wa sheria za kijinai uachane na mtazamo wa kuangalia watu wazima pekee ambao haukidhi mahitaji ya Watoto na vijana ambao

unahusisha na uwepo wa ukatili kwa Watoto; na kujenga mfumo mbadala ambapo haki za Watoto zitazingatiwa na Watoto watalindwa dhidi ya ukatili wakati wote[4].

Kutokana na matamshi hapo juu, ni ukweli usiopingika kuwa pamoja na kwamba Katiba inatoa haki za kijumla kuhusiana na maswala ya jinai kama haki ya kutokuonekana mhalifu mpaka uhukumiwe; haki ya dhamana; haki ya kupata msaada stahiki wa kisheria na haki ya kusikilizwa, na kutoa maoni, bado kuna pengo linalohitaji kujazwa hasa kuhusiana na haki za Watoto wenye kukinzana na sheria.

Tunadhani kuwa yapo masuala maalum kuhusiana na Watoto wanaoingia katika kukinzana na sheria ambayo si rahisi kuyashughulikia katika mfumo wa jinai uliopo katika Katiba ya sasa ambao unatazama na kushughulikia zaidi haki za watu wazima. Baadhi ya masuala haya maalum ni pamoja na kutazama maslahi mapana ya Watoto na ulinzi wa Watoto. Hivyo Katiba kama sheria mama ni lazima itambue vigezo hivi muhimu wakati wa kutunga ibara zinazomgusa mtoto. Kwa kufanya hivyo Tanzania itakuwa inaingiza katika Katiba kanuni muhimu zinazohusu Watoto kama zinavyotambuliwa na mikataba ya Kimataifa kuhusu Watoto.

Vilevile ni vizuri kufahamu kuwa madhumuni ya kuwa mfumo rafiki wa jinai kwa Watoto ni kuwarekebisha Watoto waliohukumiwa kwa jinai na kuwafanya wawe raia wema. Hivyo kuna tofauti kubwa sana na mfumo wa kawaida wa jinai unaolenga kumfanya mtu atubu, asifanye uhalifu tena na usiolenga katika kumrekebisha mtuhumiwa na kumbadili awe raia bora.

Ni vizuri pia kutambua kuwa vipo viwango vya kimataifa kuhusu mfumo rafiki wa jinai kwa Watoto unaotokana na mikataba mbalimbali ya Watoto. Viwango hivi vinaelekea sasa kuwa sheria za asili za kimataifa. Kwa kutambua hili nchi nyingi duniani zimeanza kuzingatia viwango hivi kama viwango ambavyo ni lazima nchi na taasisi mbalimbali katika nchi hiyo ivifikie wakati wa kutunga sheria na taratibu za kuongoza mfumo rafiki wa jinai kwa Watoto.

Tunatambua pia maboresho yaliyofanyika katika siku za karibuni kwa kufuta sheria ya zamani ya Watoto na Vijana ya mwaka 1937 (iliyorekebishwa) na kutunga Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo pamoja na mambo mengine ilianzisha Mahakama ya Watoto. Hata hivyo sheria hii mpya tayari imeonyesha kuwa na mapungufu yanayohitaji kufanyiwa kazi kama yalivyoainishwa katika kesi ya mwaka 2012 kati ya Elizabeth Michael (Lulu) dhidi ya Jamhuri.

Katika utafiti uliofanyika mwaka 2011[5] imeonekana kuwa hakuna mfumo maalum wa kuwalinda Watoto na ukatili na kudhalilishwa ikiwa ni pamoja na ukosefu wa huduma tofauti kwa wahalifu Watoto. Hali hii inahitaji matamko na nguvu za ziada kuhakikisha uwepo wa mfumo utakaohakikisha haki za Watoto zinalindwa na kuzingatiwa na wakati huohuo kuwa na mfumo

[4] Maneno haya yalitamkwa na Marta Santos Pais, mwakilishi maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayehusiki na ukatili kwa Watoto katika mkutano wa wataalamu uliofanyika Januari 2012 katika mji wa Viena ukiwa na nia ya kujadili na kukubaliana mbinu stahiki za kukomesha ukatili dhidi ya watoto wanaokabiliwa na mashtaka ya jinai.

[5] CHRAGG (2011)Inspection Report for Children in Detention Facilities in Tanzania

unaozuia uhalifu na wenye nia ya kumjenga na kumrekebisha mtoto anayetuhumiwa kwa uhalifu ili awe raia mwema.

Tunaamini kuwa kwa kuweka ibara maalum katika Katiba inayozingatia haki za Watoto walio katika ukinzani na sheria na watoto wengine wanapoingia katika mfumo wa haki wa jinai wakiwa kama watuhumiwa, waathirika au mashahidi kutajenga mazingiria yanayolenga zaidi katika kumjenga mtoto na kuweka mfumo unaolenga zaidi katika kumrekebisha mtoto na kumfanya mtoto na haki zake kama sehemu ya mchakato wa kutafuta haki za kiKatiba. Hali hii inatajarajiwa kuleta mabadiliko yatakayokuwa tofauti na matokeo ya utafiti wa UNICEF ulioonyesha kuwa watoto wanaokutana na mfumo wa sheria wa kijinai wananyayaswa na kutokutendewa haki. Inategemewa kuwa mfumo huu utakuwa chachu ya kufanya mabadiliko ya namna kesi za jinai na madai zinazowahusu watoto zinavyoendeshwa kama mchakato wa kubadilisha sheria hizi unaoratibiwa na Wizara ya Sheria na Katiba unavyoashiria.

Ni vizuri kutambua kuwa Tanzania haitakuwa ya kwanza kupitia huu mchakato maana tayari Afrika Kusini, Kenya na Uganda zimeshaupitia. Ni vizuri kufahamu pia kuwa Katiba ya Afrika Kusini inazitaja hizi haki kama haki za kulindwa dhidi ya uonevu, kukosa matunzo; pamoja na kutengwa mbali na watuhumiwa/wafungwa wenye umri mkubwa.

TCRF inapendekeza kuwepo na Katiba iliyosheheni vifungu vyote muhimu kuashiria kuwa kuna nia thabiti ya kuboresha mazingira ya kutoa huduma rafiki za kijinai kwa watoto badala ya kuhangaikia mfumo wa kizamani ambao hauko rafiki kwa Watoto na vijana.

3.6 Haki ya kulindwa dhidi ya uonevu, ukatili na udhalilishaji

Tanzania ni nchi ya pili baada ya Swaziland katika nchi za ukanda wa Sahara kufanya utafiti wa kina wa tatizo la ukatili kwa Watoto. Utafiti huu uliofanyika mwaka 2011 umeonyesha umuhimu wa kutafuta namna ya kukomesha ukatili kwa watoto. Utafiti huu ulionyesha kuwa Watoto 3 kati ya 10 walio kati ya umri wa miaka 13 na 17 wameshakutana na aina mojawapo ya ukatili uliofanywa kwao. Utafiti huu pia ulionyesha kuwa ukatili huu ulitendwa na watu walio karibu nao na wanaowaamini ambao walipaswa kuwapa huduma na ulinzi.

Ni dhahiri pia kwa sasa hakuna mfumo thabiti wa kisheria wa kulinda haki za Watoto katika Katiba yetu na sheria nyinginezo. Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 haitoi dira sahihi ya namna serikali ilivyojipanga kukomesha ukatili kwa Watoto. Hali hii inatokana na ukweli kwamba hakuna mkakati wa pamoja katika uandikaji wa sheria uliosababisha kuwepo kwa sheria nyingi bila kuwa na mfumo ulio wazi wa kuzisimamia na kuzipa meno sheria ili zilinde haki za Watoto. Baadhi ya sheria zilizotungwa karibuni ni Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 2008, Sheria ya Kuharamisha Usafirshaji wa Watu ya mwaka 2009, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 na Sheria ya Ulemavu ya mwaka 2010.

Ni dhahiri kuwa kuweka ibara zinazompatia mtoto haki zake katika Katiba kutasaidia kuboresha namna wazazi na walezi wanavyofanya mambo yahusianayo na malezi na ulinzi wa Watoto; kutoa changamoto kwenye mila na desturi kama zilivyozoeleka katika jamii zinazowaweka Watoto katika mateso zikidhaniwa kuwa ni njia muafaka za kutoa adhabu na kuimarisha nidhamu majumbani na shuleni. Pia kutawafanya watunga sera kutunga sera na programu

zinazohimiza malezi bora ya watoto yanayoweza kumjenga mtoto kama mwanajamii. Ibara hizi maalum katika Katiba zitasaidia kuweka mfumo wa sheria unaoondoa mkanganyiko unaotokana na uwepo wa sheria nyingi zinazogusa haki ya mtoto au pengine haukuweza kuondolewa na mchakato wa kutunga Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009. Vilevile uwepo wa ibara hizo utasaidia utekelezaji madhubuti wa mikakati mbalimbali ukiwamo Mkakati Mtambuka wa Kisekta wa Kukomesha Ukatili kwa Watoto.

3.8 Kuundwa kwa Taasisi Maalum ya Kuratibu, Kusimamia na kufuatilia Utekelelezaji wa Haki za Watoto Nchini .

Masuala ya watoto yamekuwa yakishughulikiwa na Wizara mbalimbali na hakuna chombo maalum chenye nguvu ya kikatiba kinachofuatilia, kuratibu na kusimamia masuala ya utekelezaji wa haki za Watoto. Kwa kuwa kumekuwa na vyombo vingi na vinafanya kazi bila kuratibiwa hii imesababisha Watoto kunyanyasika, mfano watoto wanawekwa pamoja na watu wazima magerezani na mahabusu.[6]

Uundaji wa chombo hiki cha kiKatiba utaboresha, kitafuatilia na kuratibu utekelezaji wa Haki za Watoto Tanzania. Tunapendekeza chombo kiwajibike kwa Bunge. Vilevile chombo hiki kiwe na uwakilishi wa Serikali na Asasi za kiraia.

3.9 Mfumo wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto

Nchini Tanzania hakuna mfumo wa ulinzi na usalama wa mtoto mbao ni jumuishi[7]. Tunapendekeza kuwepo kwa mfumo wa ulinzi na usalama wa mtoto ili kuhakikisha kwamba mtoto analindwa dhidi ya madhara, unyanyasaji na unyonyaji wa aina zote. Mfumo huu utawezesha Haki za Mtoto kulindwa kikatiba, kisheria, kisera, kitaasisi na kijamii. Mfumo huu utaweka vipaumbele na mikakati ya kupata rasilimali kwa ajili ya Watoto. Masuala yanayohusiana na haki na ustawi wa mtoto yazingatiwe katika ngazi zote za serikali za mtaa[8]. Utoaji wa huduma muhimu mfano afya, elimu, mavazi, malazi, chakula na usalama kwa wasio na uwezo ziwe sehemu ya mpango wa maendeleo wa ngazi husika za serikali za mitaa kama inavyoelezwa katika Sheria ya Mtoto kifungu cha 94. Jukumu hili kwa serikali za mitaa limeidhinishwa pia katika sura ya 7 ya Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008).

3.10 Kumomonyoka kwa maadili katika Jamii

Kuna mmomonyoko wa maadili na kufarakana kwa familia yaani baba mama na watoto .Mmomonyoko huu wa maadili unatokana na sababu mbalimbali zikiwemo umaskini wa kipato, utandawazi na kusahaulika kwa misingi maadili ya kitaifa. Matukio haya yanasababisha

[6] CHRAGG (2011)Inspection Report for Children in Detention Facilities in Tanzania

[7] Mfumo ambao unajumuisha sera, sheria, taasisi, huduma , rufaa na jamii katika uwajibikaji kwa ulinzi na usalama wa mtoto

[8] Mfano katika ngazi ya kitongoji, kijiji/mtaa, kata na wilaya

uvunjifu wa haki za Watoto, Watotkujua wala kutimiza wajibu wao , hali kadhalika wazazi/walezi kutoweza kutimiza wajibu wao kwa Watoto. Kwa kuwa misingi ya maadili ya taifa haifuatwi, Watoto wamekosa uzalendo na kumekuwepo na chuki baina ya matabaka ya walionacho na wasiokuwanacho katika jamii.

Umoja na ustawi wa familia ulindwe kikatiba kwa kuweka wazi kwamba familia ni msingi wa Taifa. Katiba iweke haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni ambazo zitalinda ustawi wa familia. Haki hizo ni pamoja na haki ya hifadhi ya jamii kwa watu wote hususani familia maskini. Vilevile Katiba iainishe misingi ya maadili ya kitaifa mfano: uzalendo, uadilifu, heshima, kutunza rasilimali za taifa, kumcha Mungu, kulinda amani na kufanya kazi kwa bidii.

Inaonyeshwa katika kiambatisho namba namna Katiba za nchi mbalimbali za Afrika zilivyoweza kujumuisha ibara maalum zinazoongelea haki za Watoto katika Katiba zao:

Tanzania Child Rights Forum
"together for a lasting positive change for children"
TCRF, P.O. Box 22401, Dar Es Salaam, Tanzania. Email: info@childrightsforum.org

Kiambatanisho cha Masuala muhimu yanayowahusu Watoto

Issue	**Local and International Framework**	**Best practices**	**Suggested Article**
Right to Education	The current constitution recognizes the right to education – with limitation to capacity ad enforceability.	In most constitutions the right to education is mandatory and an absolute right, while in Tanzania it remains largely the declaratory rights. In Kenya Uganda and South Africas' Constitutions this rights is stated as mandatory.	Borrow from Kenya, South Africa See art 11 of the ACRWC to define the scope) It is critical that the suggested provision should state clearly the state's obligation
Right to life and Health	***Article 25 (1) of the Universal Declaration of Human Rights (UDHR)*** UDHR Article 25 *Everyone has the right to a standard of living adequate for the health and well-being of himself and of his family, including food, clothing, housing and medical care and necessary social services.* ***Article 12 of the International Covenant on Economic, Social and Cultural Rights (ICESCR)*** Article 12	**South Africa Constitution of 1996 (Art. 28)** (1) Every child has the right, (a) to a name and a nationality from birth; (b) to family care or parental care, or to appropriate alternative care when removed from the family environment; (c) to basic nutrition, shelter, basic health care services and social services; (d) to be protected from maltreatment, neglect, abuse or degradation; (e) to be protected from exploitative labor practices; (f) not to be required or permitted to perform work or services that are inappropriate for a person of that child's age; or place at risk the child's well being…; (g) not to be detained	We recommend that this need to move from the declaratory and become mandatory as opposed to the current provision. Again, the current Constitution talks of the Social security without further elaboration. We recommend that the state's responsibility towards social security and social protection be enforced against the government as part of …..

	1. *The States Parties to the present Covenant recognize the right of everyone to the enjoyment of the highest attainable standard of physical and mental health.* *2. The steps to be taken by the States Parties to the present Covenant to achieve the full realization of this right shall include those necessary for:* *(a) The provision for the reduction of the stillbirth-rate and of infant mortality and for the healthy development of the child;* *(b) The improvement of all aspects of environmental and industrial hygiene;* *(c) The prevention, treatment and control of epidemic, endemic, occupational and other diseases;* *(d) The creation of conditions which would assure to all medical service and medical attention in the event of sickness.* ***Article 24 of the Convention on the Rights of the Child (CRC)*** Article 24 1. *States Parties recognize the right of the child to the enjoyment of the highest*	except as a measure of last resort, in which case…the child may be detained only for the shortest appropriate period of time and has the right to be – (i) kept separately from detained persons over the age of 18 years and (ii) treated in a manner, and kept in conditions, that take account of the child's age… **Kenya Constitution 2011** **53.** (1) Every child has the right— (*a*) to a name and nationality from birth; (b) to free and compulsory basic education; (*c*) to basic nutrition, shelter and health care; (*d*) to be protected from abuse, neglect, harmful cultural practices, all forms of violence, inhuman treatment and punishment, and hazardous or exploitative labour; (*e*) to parental care and protection, which includes equal responsibility of the mother and father to provide for the child, whether they are married to each other or not; and (*f*) not to be detained, except as a measure of last resort, and when detained, to be held – (i) for the shortest appropriate period of time; and (ii) separate from adults and in conditions	

	attainable standard of health and to facilities for the treatment of illness and rehabilitation of health. States Parties shall strive to ensure that no child is deprived of his or her right of access to such health care services. *2. States Parties shall pursue full implementation of this right and, in particular, shall take appropriate measures:* *(a) To diminish infant and child mortality;* *(b) To ensure the provision of necessary medical assistance and health care to all children with emphasis on the development of primary health care;* *(c) To combat disease and malnutrition, including within the framework of primary health care, through, inter alia, the application of readily available technology and through the provision of adequate nutritious foods and clean drinking-water, taking into consideration the dangers and risks of environmental pollution;* *(d) To ensure appropriate pre-natal and post-natal health care*	that take account of the child's sex and age.	

	for mothers; *(e) To ensure that all segments of society, in particular parents and children, are informed, have access to education and are supported in the use of basic knowledge of child health and nutrition, the advantages of breastfeeding, hygiene and environmental sanitation and the prevention of accidents;* *(f) To develop preventive health care, guidance for parents and family planning education and services.* *3. States Parties shall take all effective and appropriate measures with a view to abolishing traditional practices prejudicial to the health of children.* *4. States Parties undertake to promote and encourage international co-operation with a view to achieving progressively the full realization of the right recognized in the present article. In this regard, particular account shall be taken of the needs of developing* countries. ACRWC- **The Convention on the Rights of People with disabilities**		

	Article 25 - Health States Parties recognize that persons with disabilities have the right to the enjoyment of the highest attainable standard of health without discrimination on the basis of disability. States Parties shall take all appropriate measures to ensure access for persons with disabilities to health services that are gender-sensitive, including health-related rehabilitation. The UN Millennium Development Goals, especially number 4 Locally 1. The Constitution of the United Republic 1977 2. The Public Health Act, 2009 3. The persons with Disabilities Act No 9 of 2010 4. Penal code 5. The Law of the Child Act, 2009 6. The Child Development Policy(2008 Version) This policy provides for the right to life, survival and development 7. The Second National		

	Strategy for Growth and Poverty Reduction 2010-2015 (Mkukuta) Cluster III Goal number, 3, provides for: Promoting and protecting Human Rights for all, particularly for poor women, men and children, the vulnerable, including people living with HIV/AIDS Operational targets include: (i) equal access to timely justice for all (ii) social, political, economic and cultural rights for all particularly vulnerable groups ensured (iii) children rights promoted and protected		
Right to a identity (Name and nationality)	CRC art 7, ICCPR art 24 (2) and (3) UDHR ACRWC art 6	Uganda:**Constitution of 1995 (Art. 34)** Subject to laws enacted in their best interests, (1) children shall have the right to know and be cared for by their parents or those entitled by law to bring them up; (2) A child is entitled to basic education which shall be the responsibility of the state and the parents of the child; (3) No child shall be deprived by	It is proposed that the unlike Kenya, the registration of births be made more explicit by applying the wording of the ACRC . Every child shall have the right from his birth to a name 2. Every child shall be

	Birth and Death Registration Act, Cap 108 Citizenship Act 1995 The Law of the Child Act 2009 National Birth Registration Strategy for the Under Five. Global Commission on Accountability on child and Maternal Health	any person of medical treatment, education or any other social or economic benefit by reason of religious or other beliefs; (4) Children are entitled to be protected from social or economic exploitation and shall not be employed in or required to perform work that is likely to be hazardous or to interfere with their education or to be harmful to their health or physical, mental, spiritual, moral or social development; (5) ….of clause (4) of this article, children shall be persons under the age of sixteen years; (6) A child offender who is kept in lawful custody or detention shall be kept separately from adult offenders; (7) The law shall accord special protection to orphans and other vulnerable children. **Kenya Constitution :** **14** (4) A child found in Kenya who is, or appears to be, less than eight years of age, and whose nationality and parents are not known, is presumed to be a citizen by birth. **53.** (1) *Every child has the right—* *(a) to a name and nationality from birth;* (b) to free and compulsory basic education; (*c*) to basic nutrition, shelter and health care; (*d*) to be protected from abuse, neglect, harmful cultural practices, all forms of violence, inhuman treatment and punishment, and hazardous or exploitative	registered immediately after birth. 3. Every child has the right to acquire a nationality However, we believe that given Tanzania current set up- nationality is subject to different treatment which we are sure will feature through different consultations. However, in relation to a child- consideration must be given to the fact that children should not be stateless and the mischief sought to be addressed by the CRC must be observed, in which case it is suggested that we adpt Kenya example where by children will be considered of Kenya nationality as per at art **14** (4*) A child found in Kenya who is, or appears to be, less than* *eight years of age, and whose nationality and parents are not known, is* *presumed to be a citizen by birth.* N (recommend we follow Kenya example and then strengthen the protection of this right). See also how we can separate the discussion on the identity and the nationality and take up identity as one basic minimum)

		labour; (*e*) to parental care and protection, which includes equal responsibility of the mother and father to provide for the child, whether they are married to each other or not; and (*f*) not to be detained, except as a measure of last resort, and when detained, to be held – (i) for the shortest appropriate period of time; and (ii) separate from adults and in conditions that take account of the child's sex and age. (2) A child's best interests are of paramount importance in every matter concerning the child. **Malawi:** **Constitution of 1994 – most recent amendment 2001 (Art. 23)** (1) All children, regardless of the circumstances of their birth, are entitled to equal treatment before the law; (2) All children shall have the right to a given name and a family name and the right to a nationality; (3) Children have the right to know, and to be raised by, their parents; (4) Children are entitled to be protected from economic exploitation or any treatment, work or punishment that is, or likely to be hazardous; interfere with their education; or	

		be harmful to their health or to their physical, mental or spiritual or social development; (5) For the purposes of this section, children shall be persons under sixteen years of age **South Africa:** **Constitution of 1996 (Art. 28)** (1) Every child has the right, (a) to a name and a nationality from birth; (b) to family care or parental care, or to appropriate alternative care when removed from the family environment; (c) to basic nutrition, shelter, basic health care services and social services; (d) to be protected from maltreatment, neglect, abuse or degradation; (e) to be protected from exploitative labour practices; (f) not to be required or permitted to perform work or services that are inappropriate for a person of that child's age; or place at risk the child's well being…; (g) not to be detained except as a measure of last resort, in which case…the child may be detained only for the shortest appropriate period of time and has the right to be – (i) kept separately from detained persons over the age of 18 years and (ii) treated in a manner, and kept in conditions, that take account of the child's age…	
Right of Opinion (Child Participation	In the LCA it is not very clear and very scattered… we need to		We may need to premise this on

)	have a harmonized provision. Art 18 of the Constitution is more generic with no specific mention to children.		CRC.
Juvenile justice	• *The United Nations Standard Minimum Rules of the Administration of Juvenile Justice (the Beijing Rules),* • *The United Nations Guidelines for the Prevention of Juvenile Delinquency (Riyadh Guidelines),* • *The United Nations Rule for the Protection of Juveniles Deprived of their Liberty (UNRPJ),* • *The United Nations Standard Minimum Rules for Non Custodial Measures (Tokyo Rules),* • *The United Nations Guidelines for Action on Children in the Criminal Justice System,* • *The United Nations*	**South Africa:** **Constitution of 1996 (Art. 28)** (1) (g) not to be detained except as a measure of last resort, in which case…the child may be detained only for the shortest appropriate period of time and has the right to be – (i) kept separately from detained persons over the age of 18 years and (ii) treated in a manner, and kept in conditions, that take account of the child's age… **Kenya Constitution :** **14** (*f*) not to be detained, except as a measure of last resort, and when detained, to be held – (i) for the shortest appropriate period of time; and (ii) separate from adults and in conditions that take account of the child's sex and age. (2) A child's best interests are of paramount importance in every matter concerning the child. **Uganda's Constitution of 1995 (Art. 34)** Subject to laws enacted in their best interests,….. (5) ….of clause (4) of this	

	Declaration of Basic Principles of Justice for Victims of Crime and Abuse of Power. • *CRC Committee General Comment No 10 of 2007* *United Nations Guidance Note of the Secretary General: UN-approach to Justice for Children, September, 2008* *The Law of the Child Act*	article, children shall be persons under the age of sixteen years; (6) A child offender who is kept in lawful custody or detention shall be kept separately from adult offenders; (7) The law shall accord special protection to orphans and other vulnerable children.	